# SOMO: SAYANSI NA TEKNOLOJIA.

**SEHEMU: A (ALAMA 20)**

MsomiBora.com

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

**(i)** **(i)** Mwalimu aliwaambia wanafunzi wa darasa la tano waoredheshe wanyama wasio na uti wa mgongo kundi la anthropoda je? Ni kundi lipi kati ya makundi waliyo orodhesha lilikuwa sahihi **A**.Kaa,Panzi na Buibui **B**.Panzi, Minyoo na Kaa **C**.Konokono,Jongoo na Ngisi **D**. Konokono,Ngisi na Nyungunyungu **E**.Nyungunyungu,Ngisi na Buibui

**(ii)** Bibishamba aliwaelezea wakulima kuwa udongo wa mahali hapa haufai kwa kilimo,utwamisha maji wakati wa masika na nyakati za kiangazi huwa ngumu sana.Je? Udongo wa eneo hilo ni udongo wa aina gani? **A**.Kichanga **B**.Tifutifu **C**.Mfinyanzi **D**.Tifutifu na Kichanga **E**.Wenye mboji

**(iii)** Alama za usalama ni alama ambazo hutoa taarifa kuhusu hatari iliyopo kwenye vitu au mazingira.Je? Alama za lazima au Amri huoneshwa kwa rangi ipi? **A.**Njano B.Nyekundu **C**. Bluu **D**.Kijani **E**.Nyeupe

**(iv).**Wanafunzi wa darasa la sita walifundishwa kuhusuhewa mbalimbali zilizopo katika Anga hewa je?Ni hewa ipi hutumika katika usindikaji wa vyakula? **A**.Oksijeni **B**.Kabonidioksaidi **C**.Naitrojeni **D**.Haidrojeni **E**.Kabonimoksaidi

**(v).**Babu alimunyoa mdogo wangu kwa kutumia mkasi.Je? unafikiri mkasi ni aina gani ya mashine? **A**.Mashine tata **B**.Mashine nyepesi **C**.Mashine sahili **D**. Wenzo **E**. Mashine bora

**(vi).**Rehema husumbuliwa na homa za mara kwa mara,kutokwa na damu sehemu za wazi za mwili kama vile machoni,puani na masikioni.Unafikiri Rehema anasumbuliwa na ugonjwa gani? **A**.Ukimwi **B**.Kipindupindu **C**.Pangusa **D**.Matende **E**.Ebola

**(vii).**Mkondo wa umeme wa ampia 0.6 umepita katika waya wenyeukinzani wa Ohm 20. Tafuta tofauti ya potenshali katika waya **A**.Volti 20 **B**.Volti 20.6 **C**. Volti 12 **D**.Volti 19.4 **E**. Volti 120

**(viii).**Mwalimu anahitaji kuandaa matokeo ya mtihani wa darasa la saba.Ni programu gani katika tarakilishi ataitumia kufanya kazi hii **A**.Programu jedwali **B**.Programu andishi **C**. Programu tumizi **D**. Visakuzi **E**.Kingavirusi

**(ix)**Afisa kilimo alielimisha jamii kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa,wewe kama mwanafunzi wa darasa la saba,unafikiri ni aina gani ya antenna inatumika kupokea mawimbi ya taarifa ya mwenendo wa hali ya hewa? **A**.Yagi-Uda **B**. Antena honi **C**.Antena kitanzi **D**. Dishi **E**.Antena kidoa

**(x).**Jiwe lina uzito wa N100 likiwa hewani.Ikwa jiwe hilo limezana kwenye ugiligili uzito wake ni Newton 80.Tafuta kanielezi inayosukuma jiwe hilo. A. N 20 B.N 180 C.N 800 D.N 100 E. N 120

**2.Oanisha sehemu A na sehemu B ili kupata maana sahihi kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.**

| SN | SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|---|
| i | Tindikali | A.Milango ya fahamu |
| ii | Mboga za majani na matunda | B.Dawa ya kuua wadudu waenezao magonjwa |
| iii | Mfumo wa upumuaji | C.Kubadili karatasi ya litimasi bluu kuwa nyekundu |
| iv | Neva za uoni | D.Pua,Koromeo,trakea,mapafu |
| v | Viuatilifu | E.Kulinda mwili dhidi ya magonjwa |
| | | F.Kupeleka taarifa kwenye mfumo wa kati wa fahamu |

**3.**Jaza nafasi zilizo wazi ili kuamilisha vipengele vifuatavyo

**(i)** Kitu kikizama kiasi ama chote kwenye ugiligili kinapata ukinzani wa……………………………………………………………ambayo ni sawa na uzito wa ugiligili uliohamishwa na kitu hicho.

**(ii)** Mashine tata huundwa na…………………………………………………………………….. zaidi ya moja.

**(iii)** Gesi vunde,upepo,joto ardhi, mawimbi ya maji na maporomoko ya maji ni mfano wa aina gani ya nishati…......

**(iv)** Kuyeyuka kwa barafu ni badiliko la………………………………………

**(v)** Kunawa maji tiririka,kuvaa barakoa,kuepuka msongamano ni miongoni mwa tahadhariza kuepuka ugonjwa wa………………………………………………………

**SEHEMU B(ALAMA 20)**

**4.Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika jibu fupi**

(i)Amina ana mtoto mwenye ualibino. Hali hiyo imesababishwa na ngozi kukosa nini………………………………………….

(ii) Njia maalum ya umeme huitwaje?..............................................................

(iii)Shule ya msingi Mtakuja wamejenga sehemu maalum inayotumika kuteketeza taka kwa kutumia joto kali. Je sehemu hiyo inaitwaje?..........................................

**5.(**i) Nini hutokea mwale wa mwanga unapopita kwenye midia mbili tofauti………………………………………
(ii) Nini hutokea iwapo densiti itakuwa kubwa kuliko density ya maji?..................................................
(iii) Bwana Juma anafanya kazi ya ukuli wewe kama mwanasayansi utamshauri atumie chakula cha aina gani kwa wingi……………………………………………..


6.(i) John na Moses ni marafiki kila mara wakikutana hubisha kuhusu VVU na UKIMWI wakisema hakuna umuhimu wa kupima VVU na UKIMWI.Wewew kama mwanafunzi wa darsa la saba utwashauri nini?

(ii) Mwalimu wa darasa la saba anataka kuandaa kadi za mwaliko kwa ajili ya mahafali ya darasa la saba.Je? utamshauri atumie program gani katika kompyuta?

(iii) Wanafunzi walipewa kazi ya kutengeneza antenna.je?ni hatua ipi ya kwanza ya kuzingatia katika utengenezaji wa antena?

(iv) Juma alipewa kazi na mwalimu wake wa sayansi kutafuta densiti ya chupa.je? ili apate densiti ya chupa hiyo anapaswa kutumia kanuni ipi?

7.(i) Tafuta thamani ya x katika mcoro ufuatao.




(ii) Matendo ya hiari huratibiwa na sehemu ipi ya ubongo?

(iii) Jengo moja karibu na shule ya msingi Matapa ilishika moto,kabla ya jingo kuungua sana kikosi cha zima moto walifika na kufanikiwa kuuzima. Je? Unafikiri kikosi cha zima moto walitumia gesi ya aina gani kuuzima moto huo?

(iv) Mbuzi ni mmojwapo wa wanyama wanoishi kwa kula mimea,je? Wanyama wanaishi kwa kutegemea kula mimea wanaitwaje?

8.

MsomiBora.com

# SOMO: URAIA NA MAADILI.

.

1. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi hiyo.

(i) Jukumu la kuwasaidia watu wenye mahitaji katika jamii ni la …………….
(A) Wanafamilia (B) Wanajamii? (C) Serikali na wanajamii wote(D) Taasisiza dini (E) Ukoo.

(ii) Uhuru wa kujielezea ni sifa ya demokrasia . Je, huhusisha shughuli zipikati ya zifuatazo………….. (A) Uwazi (B) Uchaguzi huru na wa haki (C) Uhuru wa kutoa maoni (D) Ushirikishwaji (E) Kujiunga kwenye vyanma vya siasa.

(iii) Ifuatayo ni faida ya kuwahudumia watu wenye uhitaji katika jamii isipokuwa ………(A)Kujenga upendo (B) Kudumisha udugu (C) Kuthamini utu (D) Wizi (E) kulinda haki za binadamu.

(iv) Madhara ya matumizi mabaya ya vyombo vya habari ni pamoja na ……….(A) Kuleta maendeleo (B) Kuelimisha jamii (C) Kuleta chuki, taharuki na mapigano katika jamii (D) Kudumisha amani katika jamii (E) Kuleta na kudumisha usawa wa kijinsia.

(v) Ipi kati ya zifuatazo si njia inayoweza kutumika kuitangaza Tanzania? …….. (A) Maonesho ya biashara (B) Matangazo atika vyombo vya habari (C) Mahubirio ya dini (D) Michezo mbalimbali (E) Utamaduni.

(vi) Jukumu la kulinda raia na mali zao hapa Tanzania ni la nani ? (A) Jeshi la polisi (B) Wananchi (C) Wanakijiji wote (D) JKT (E) JWTZ.

(vii) Kila shule ina uongozi wake ambao hupatikana kwa njia ya kuchaguliwa na wengine kuingia kwa nyadhifa zao. Je, katibu wa vikao vya kamati ya shule ni…….. (A) Mwenyekiti (B) Mwalimu mkuu (C) Mwalimu wa nidhamu ?(D) Mwalimu wa taaluma (E) Kiranja mkuu.

(viii) Mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania ulirejeshwa mnamo mwaka 1992. Vyama hivyo vya siasa vilishiriki mwaka gani katika uchaguzi mkuu kwa mara ya kwanza ?……. (A) 1995 (B) 1999) (C) 2000 (D) 2002 (E) 1967.

(ix) Lipi kati ya majibu yafuatayo si faida ya uvumilivu ? Kujenga busara (B) Kujenga hofu (C) Kuchochea utulivu wa akili (D) Kufanya uamuzi sahihi (E) Kusababisha ghasia katika jamii.

(x) Maarifa na stadi za kuendesha na kusimamia uhusiano wa kimataifa hujulikana kama …………(A) Diplomasia (B) Demokrasia (C) Wajibu (D) Haki (E) Uwajibikaji .

2. (i). Oanisha fungu A na fungu B ili kuleta maana sawa.

| FUNGU A | | FUNGU B |
|---|---|---|
| (i) | Utamaduni. | shi kupata elimu, maji na huduma za afya. |
| (ii) | Mihimili ya dola. | mbukumbu ya muungano. |
| (iii) | Kukuza ubunifu. | umuisha lugha , sanaa, mavazi na imani. |
| (iv) | 26/04/ kila mwaka. | hakama , Bunge na Serikali. |
| (v) | Haki za binadamu. | kelezaji wa mpango katika maisha. |

| FUNGU A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| FUNFU B | | | | | |

3. Jaza nafasi zilizoachwa wazi.

A. Ni tukio gani la kihistoria ambalo halitasahulika hapa Tanzania lililotokea machi 2021_______________.
B. Jeshi la zimamoto na uokoaji hapa Tanzania lilianzishwa mwaka _____________.
C. Dunia imekuwa kama kijiji kimoja hii ni kutokana na utandawazi na kutokana na kuttaarifa na kupokea kitaifa na kimataifa . Je, njia hizo huuitwaje? _____________ .
D. Nchini Tanzania muhimili wa dola unaohusika na kutafsiri na kusimamia kutoka Bungeni huitwa?_______________.
E. ____________ ni fedha au kitu cha thamani kinachotoiewa na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo Fulani ili mtoaji apate upendeleo .

4. Panga sentensi zifuatazo kwa mpangilio sahihi kwa kuipa herufi A,B,C,D na E

(i) Sensa ya watu na makazi ijayo itafanyika mwaka 2023.
(ii) Nchini Tanzania sense ya watu na makazi hufanyika kila baada ya miaka 10.
(iii) Sensa ni mchakato wa kuhesabu watu , nyumba na mifugo.
(iv) Sensa ya watu na makazi kwa mara ya mwisho nchini ilifanyika mwaka 2022.
(v) Serikali hufanya mchakato wa sense kwa lengo la kutoa huduma kwa watu wake kwa usahihi.

5. Jaza nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Bendera ya Taifa la Tanzania ina jumla ya rangi nne. Rangi ya njano katika bendera ya Taifa huwakilisha__________________.
(ii) Kwa kawaida mkuu wa mkoa huwa na mshauri wake ambaye huteuliwa na Rais. Mshauri wa mkuu wa mkuu wa mkoa ni ________________.

(iii) Mapendekezo ya maandishi ambayo huwasilishwa kwa Rais baada ya kujadiliwa na bunge la jamuhuri ya muungano wa Tanzaniaq hujulikana kama________________.
(iv) Katika utamaduni wa Tanzania kila kabila ina utamaduni wake. Ni ngoma gani ya asili inayochezwa na watu wa jamii ya Wahaya?_______________.
(v) Kwa kawaida watu huolewa bna kuoana .Kundi la watu lenye uhusiano wa kinasaba hujulikana kama_____________.

6. Soma kifungu cha habari ifuatayo kisha jibu maswali kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Jamhuri ya muungano wa Tanzania ni muunganiko wa nchi mbili huru.Nchi izo ni Tanganyika na Zanzibar .Tanganyika iliongozwa na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye aliwaongoza wananchi kupigania Uhuru wa Tanganyika.Tanganyika ilipata uhuru wake tarehe 9/12/1964. Chama kilichoisaidia Tanganyika kupata uhuru wake ni Tanganyika African Nation Union (TANU). Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa waziri mkuu wa kwanza wa Tanganyika.

Zanzibar iliongozwa na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume ambaye aliwaongoza wananchi wa Zanzibar kupigania uhuru wao kutoka kwa utawala wa Sultani. Uhuru wa Zanzibar ulipatikana kwa mapinduzi yaliyofanyika tarehe 12/01/1964 kupitia chama cha Afro shirazi Party (ASP).Baada ya kupata uhuru nchi hizi mbili ziliungana tarehe 26/04/1964. Nchi hizi ziliunda jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais wa kwanza wa Tanzania akawa Julius Kambarage Nyerere na makamu wa Rais akawa Sheikh Abeid Amani Karume.

**Maswali**.

(i) Nchi ya Tanganyika na Nchi ya Zanzibar ziliungana kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka____________.
(ii) Waziri mkuu wa Kwanza wa Tanganyika alikuwa ni _____________.
(iii) Chama kilichopigania uhuru wa **Tanganyika** kilikuwa ni ___________.
(iv) Makamu wa Rais wa Jamhuri yan Muungano wa Tanzania na Rais wa serikali ya mapinduzi wa Zanzibar alikuwa ni _____________.
(v) Jina Tanzania lilianza kutumika rasmi mwaka______________.

# ENGLISH – LANGUAGE

This paper consist of sections A,B and CWITH SEVEN QUESTIONS AND THIRTY FIVE ITEMS.

SECTION A.

LISTENING,MULTIPLE CHOICE,MATCHING ITEMS AND FILL IN THE BLANK.

1. (i) One of the food crop grown by the family is
   A.Cothes B. Animals C.Cassava D. Goat E.Domestic use

   (ii) Neema and Justa are……………………..daughters.

   A. Ajuna's B.Paul's C.Petro's D.Neema's E.Jane's

   (iii) The four children's grandfather is…………………

   A.Paulo B. Petro C. John C.Ajuna E. Neema

   (iv) One among the the following is not a domestic use sold in the shop

   A.Soap B. Sugar C. Farm D.Cooking oil E.Rice

   (v) Ajuna will sit for her standard seven national examination in………………….

   A. 2025 B. 2026 C. 2027 D. 2028 E. 2029

2. (I) Our young sister………………………her arm last year.

A. Will broke B. Brroked C. Break D. Broke E. Breaking ( ).

(i) I shall……………my national examinational next year.

A.Did B. do C. done D.did E. have do.

(iii) Juma and Anna……….desided to stop attending to school.

A .were B.was C. have D.has E. will.

(iv) I…………to school every day.

A. Go B. went C. gone D. going E. goes.

(v) Joseph was reading while his uncle…………………TV.

A. is watching B. were watching C. was watching D. are watching E. does watch.

3. GRAMMAR: choose the correct word from the brackets below.

(i) What is the meaning of the prefix "pre" in the word pre-national?

(before, after, besides).

(ii) She is more beautiful than a moon and stars, what figure of speech in this statement?

(simile, metaphor, hyperbole).

(iii) All the passengers got off the bus……………John.

(only, except ,for).

(iv) The man ………………you are talking about is in the office.

(who, whose, whom).

(v) Thomas has car ……………..car is very fast.

(Thoma's, Thomas's, Thomas')

4. VOCABULAR :(match the items of group A with those of group B by writing a letter of the correct answer).

| S/N | GROUP A | ANSWER | GROUP B |
|---|---|---|---|
| (i) | Piglet | | A).The first meal in the morning |
| (ii) | Pedestrian | | B).A young lion |
| (iii) | Cub | | C).A person who treates sick people. |
| (iv) | Doctor | | D).A young pig. |
| (v) | Dinner | | E).A person who walks on foot. |
| | | | F). A person who takes care of sick people. |
| | | | G). A young goat. |
| | | | H). A meal eaten in the evening. |

**SECTION B**: Fill in the blanks.

5(i) A month before June is called……………….

(ii) The father of your father or Mother is……………..

(iii) A week consists………………days.

(iv) A plural of the word sheep is……………………….

(v)……………..is the book that consists of alphabetical list of words with their meaning.

6. **READING**: Ready the below passage and then answer question I……………v

Irene and Morine are twins. They live in Kyela. They are in class three at Kajunjumile primary school. Their sisters Eliza is in class five at Kitunge primary school. It is a boarding school.

One day Irene and Morine decided to write a letter to their sister. They wanted to tell her about their progress in studies.

**QUESTIONS.**

(i) What are the twins name?
(ii) What is their sisters name?
(iii) Where do they twins live?
(iv) What is the name of their school?
(v) What is Eliza's school nam ?

**SECTION C:(JUMBLED SENTENCES**).

Re__arrange the below sentences in a correct order by giving them letters A,B,C,D and E.

(i) John was very happy because he had passed the examinations.
(ii) He wanted to see his exams results
(iii) First he looked at the paper on the school noticeboard.
(iv) John ran to the school.
(v) He ran home to tell his parents.

**LISTENING SKILLS**.

Mr John Paul has four children .His wife is Jane. The first born is Neema and the last one is Ajuna who is in class three this year. Other children are Justa and Petro.This family grows beans, maize, cassava, and bananas. They also keep animals such as goats, cows and dogs. This family has a big shop where domestick uses are sold.

# KISWAHILI

KIFUNGU CHA HABARI CHA KUSIKILIZA

SEHEMU A. UFAHAMU WA KUSIKILIZA.

Maji ni moja kati ya vitu vitatu muhimu vinavyotuwezesha kuishi. Vingine ni hewa na chakula. Kila mtu anaelewa umuhimu wa maji katika maisha ya viumbe hai, baadhi ya viumbe hai kama vile Samaki, Mamba, na Konokono maskani yao ni majini, Hivyo maji yakikosekana, viumbe hao huweza kuaga dunia.

Binadamu hutumia maji kwa shughuli mbalimbali kama vile kupika, Kufua, na Kunywa.

**MASWALI**

I. Binadamu hutumia maji kwa shughuli zipi? Kutokana na kifungu cha habari ulichosoma.
A: Kupika, Kuoga na kunawa. B: Kuoga, Kupika, Kufua na kunywa C: Kuchemsha, Kunywa, Kufua na Kuoga D: Kudeki, Kufua, na Kunywa E: Kuosha vyombo, Kuishi, Kunawa na Kunywa

II. Neno maskani kama lilivyotumika katika habari humaanisha nini?
A: Mazingira B: Nyumbani C.Majini D: Viumbe hai E. Maisha.

III. Vitu muhimu katika maisha ya Binadamu ni.
A: Maji, hewa, na chakula B: Chakula, Hela na hewa C:Chakula, Mavazi na Hela E: Maji, Chai na Mazingira.

IV. Kichwa cha habari kinafaa kiwe
A:Umuhimu wa Viumbe hai. B: Maskani ya viumbe hai C: Umuhimu wa Maji D: Matumizi ya Maji E: Mahitaji muhimu.

V. Mamba, Samaki, na Konokono viumbe hivi huishi wapi?.
A: Ardhini B: Hewani C: Nyumbani D: Majini E: Shambani.

SWALI LA PILI.

2. Chagua herufi yenye jibu sahii kasha iandike kwenye kisanduku.

I. Katika Zahanati ya kijiji chetu wanatibu homa, Kikohozi, Kuhara na Kaswende. Hivyo Zahanati hiyo wanatibu…………( ).
A. Matibabu B. Magojwa C. Kaswende tu D. Nafaka E. Vitu.

II. Baba alinilipia ada ya Shule. Ni neon gani linaweza kutumika kama mbadala wa neno **ada**? ( )
A. Posho B. Nauli C. Karo D. Kero E. Rambirambi.

III. Mwalimu Mtoro aliadhibiwa na Mwalimu wa darasa. Neno mtoro limetumika kama aina gani ya maneno? ( )
A. Kielezi B. Nomino C. Kitenzi D. Kiwakilishi E. Kivumishi

IV. Katika maisha hatutakiwi kufuata mkumbo. Bainisha kiambishi cha mkanushi kilichopigiwa mstari ( ).
A. –taki- B. ha- C. –iwi- D. –tu- E. –aki-

V. Neno kiai lipo katika ngeli ipi?( )
A. A-WA B. I-KI C. KI-VI D. I-ZI E. LI-YA

VI. Tungeliwahi kuamka………. Usafiri kwa urahisi . Kamilisha sentensi hii ( )
A. Tungelipata B. Tungepata C. Tungapata D. Tukipata E. Tungalipa.

VII. Katika neno wataimba kiambishi kinachoonesha wakati ni ( ).
A. –TA- B. –WA- C. –BA- D. –IMBA- E. –MBA-

VIII. Mbuzi huyu anakunywa maji. Andika wingi wa sentensi hii.
A. Mbuzi huyu anakunywa maji. B. Mbuzi hawa anakunywa maji C. Mbuzi huyu anakunywa maji D. Mbuzi hawa wanakunywa maji E. Mbuzi hii inakunywa maji.

IX. Bata na kuku wanadonoana. Sentensi hii ipo katika kauli gani? ( )
A. Kutendeana B. Kutenda C. Kutendeka D. Kutendesha E. Kutendana.

X. Ng'ombe dume aliyehasiwa huitwa…………( ).
A. Fahali B. Fahari C. Ndama D. Mbuguma E. Maksai

3. Oanisha maneno ya sehemu A na sehemu B katika jedwali lifuatalo

| SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|
| i) Maana ya nahau Zaa Matunda ni | a. Marejeo ng'amani |
| ii) Bega kwa Bega | b. Maboga |
| iii) Mwenda tezi na omo | c. Akiba haiozi |
| iv) Watoto wa tajiri wa nguo wanatembea uchi | d. Fanya kazi kwa pamoja |

| | |
|---|---|
| v) Weka akiba kwa maslahi ya badae | e. Fanya kwa uvivu |
| | f. Pata faida |
| | g. Fuja mali. |

4. Zipange sente hizi ili zilete mtiririko wenye maana kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E.

(I). Baba alinyanyuka haraka na kuelekea kule sauti ilipokuwa inatokea (   ).

(II). Ilikuwa ni siku ya Jumamosi majira ya sa saba na robo usiku (   ).

(III). Ghafura ikasikika sauti ya kilio kutoka katika moja ya vyumba pale ndani (   ).

(IV). Wakati huo tulikuwa tumeshakula chakula cha usiku na tulikuwa tumeketi sebuleni tunasikiliza taarifa ya habari (   ).

(V). Kumbe alikuwa ni mdogo wangu amebanwa na Mlango (   ).

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kasha jibu maswali yafuatayo.

Yasafishe masikizi, Ubongo uwe timamu
Shuleni uchape kazi, Pamoja nao hirimu
Kubaki kwenye gonezi, Dunia takudhulumu
Maisha huwa magumu, kukaa bila elimu.

Mtindo wa siku hizi, Kusoma na kufahamu,
Soma sifanye ajizi, Elimu kwetu ni chumu,
Una akili tambuzi, Daima uiheshimu
Maisha huwa magumu, Kukaa bila elimu.

**MASWALI**

I. Katika ubeti wa kwanza mwandishi ametumia neno hirimu ambalo kisawe chake ni…...
II. Shairi hili lina jumla ya beti ngapi ?......................
III. Vina vya kati ni…………..na vya mwisho ni……………………..
IV. Je ni ipi ni mkarara wa shairi hili?........................
V. Mshoro wa pili katika ubeti wa pili unayo mizani mingapi?..................

**6.Kamilisha utunzi wa Barua ifuatayo hapa chini kwa kujaza sehemu zilizowazi.**

Kiji cha Songambele,
S.L.P 230
KYERWA
(I)……………………………

M/Kiti wa kijiji Kaisho.
(II)……………………………
KYERWA.

(III)……………………………………………………………………………

Kichwa cha barua hapo juu cha husika.

Kutokana na maazimio ya mkutano mkuu wa kijiji ya kujenga barabara. Mimi Fidelis Mtakyamirwa Afisa Mtendaji wa kijiji cha Songambele ninakubali kushirikiana na Wanakijiji wenzangu katika ujenzi wa barabara hadi kufanikisha zoezi hilo.

(IV)………………………………..

Wako katika maendeleo ya kijiji chetu

(V)…………………………………..
Afisa Mtendaji wa Kijiji.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA.**

**MTIHANI WA MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI**

**DARASA LA SABA 2024**

SEHEMU “A” (ALAMA 20).

1) Chagua herufi ya jibu sahihi.

i. --------- ni jumla ya mambo yote yanayyomzunguka binadamu.

a). Mistu b) Mazingira c) Makazi d) Milima.

ii. Ni hali ya ukosefu wa mvua zinazotegemewa kwa miuda mrefu

a) Hali joto b). Ukame c). Kimbunga. d ). Hali ya hewa e). Tabianchi

iii. Ni aina ipi ya madini ambayo hupatikana zaidi katika mikoa ya Geita na Shinyanga.

a). Shaba b) Chumvi c). Dhahabu d). Chuma e). Rubi.

iv. Amosi alipima umbali kwenye ramani na kupata SM 10.5, endapo kipimo cha ramamni hiyo ni 1: 50,000, kokotoa umbali huo katika ardhi.
a). 10 km b). 525 km c). 5 km d). 5.25km e). 5.75 km

v. Uchaguzi Mkuu wa Vyama vingi vya siasa katika Tanzania ulifanyika, mwaka 1995. Je ni Rais yupi kwa mara ya kwanza alianza na mfumo huo.

a). JK. Nyerere b). A.H.Mwinyi c). B. W.Mkapa
d). J.P. Magufuli e) S.S.Hassani.

vi. Mwalimu wetu alitufundisha matukio mbalimbali ya kihistoria katiaka nchi yetu, mojawapo kati a hayo ni kuvumbuliwa kwa fuvu la binadamu wa kale lililotokea huko ----------------------- a). Kondoa b). Bagamoyo c). Ismila
d). Oldvai e). Engaruka.

vii. Njia mojawapo ya Tanzania kupanga njia sahihi ya maendeleo ni kufahamu idadi ya watu wake ipi ni sahihi ya kupata idadi ya watu katika eneo fulani.
a). kufanya mkutano b) Kuwaandikisha watu katika vyama vya siasa.
c). Kufanya sense ya watu na makazi. d. kusajili idadi ya watoto wanaozaliwa nchini. e. Kusajili idadi ya vifo vya watoto nchini.

viii. Zifuatazo ni athari za tetemeko la ardhi isipokuwa.
a). Uhalibifu wa mazingira na makazi kwa viumbe hai.
b). Mlipuko wa Magojwa. C). Kuongezeka au kupungua kwa kina cha bahari. D). Nyasi kukua kwa haraka shambani e). kifo kwa viumbe hai

ix. Redio D.W ya Ujerumani hutangaza taarifa ya habari saa 7:00 mchana hapa Tanzania, wakati saa za Tanzania huhesabiwa kwenye longitude ya $45^0$ Mashariki, wakati huo Ujerumani inamakuwa saa 5:00 Asubuhi. Je saa za Ujerumani huhesabiwa kwenye Longitudo ipi.
a). $75^0$ Mashariki b). $15^0$ Mashariki c). $75^0$ d). $15^0$ Magharibi
e). $30^0$ Mashariki.

x. Binadamu wa sokwe ni jamii inayofanana kiasi. Je ni nini kilimtofautisha binadamu wa kale a sokwe. a). Aina za Vyakula walivyokula b). Uwezo wa kubuni, kutengeneza na kutumia zana. C ). Ukubwa wa vichwa d). Mazingira waliyoishi e). Uhodari katika kutafuta chakula.

xi. Moja kati ya maelezo yafuatayo SIKWELI kuhusu dunia
a). Ni ya tatu kutoka kwenye jua. b). Sayari pekee yenye Mimea ya Kijani c). Ni ndogo kuliko jua. d ). Viumbe haviishi juu yake.
e). Sehemu kubwa imefunikwa kwa maji.

xii. Kilimo ni uti wa mgongo katika uchumi wa Taifa letu. Je ni Mikoa ipi zao la pamba hustawi kwa wingi. a ). Dodoma na Singida b ). Iringa na Mbeya
C ). Mwanza na Shinyanga d). Dar es Salaam na Tanga e ). Ruvuma na Mtwara.

xiii. Rehema anataka msaada wako kumwezesha kujibu swali kuhusu dhana ya utamaduni. Je ni vielelezo vipi vya utamaduni utakavyompa Rehema ili aweze kuelewa vizui dhana hivyo?
a ). Lugha, Mila, na Tohara b ). Mila, desturi na Miiko c ). Mila, desturi na Lugha
d ). Tohara, Mila, desturi e ). Lugha, Mila na Makumbusho.

xiv. Jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki ilianzishwa mwaka.
a ). 1967 b ). 2005 C ). 1965 d ). 1961 e ). 1964

xv. Ili kuongeza kipato na kufaidi matunda ya ujasiliamali ni vyema.
a ). Kufanya kazi kwa bidii b ). Kupumzika na kusubili mapato
c ). Kuomba msaada wa Mungu. d ). Kutafuta watumiaji. e ). Kutafuta ushauri.

2) Oanisha maneno ya Safu A na Safu B kisha andika majibu yako kwa kujaza herufi sehemu ya majibu.

SAFU A

| | | |
|---|---|---|
| I. Anemomita | a. | Hupima ukubwa wa tetemeko la ardhi |
| II. Upepo | b. | Mojawapo ya faida za upepo |
| III. Kuwezua mapaa | c. | Hupima mgandamizo wa upepo |
| IV. Kuchavusha mimea | d. | Hupima joto la mahali |
| V. Sesimomita | e. | Hurutubisha mimea |
| | f. | Hupima kasi ya upepo |
| | g. | Hewa inayokwenda kwa kasi |
| | h. | Upepo uvma kwa kasi |
| | i. | Mojawapo ya hasara za upepo. |

SEHEMU B ( ALAMA 20 ) JAZA NAFASI WAZI

3) Jaza nafasi wazi

i. Utando mithiri ya blanketi unaofunika uso wa dunia usipiwe moja kwa moja na miale ya jua ni ___________________________

ii. Ni aina gani ya anga ambayo huakisi mawimbi ya redio hiyo kuwa muhimu sama katika mawasiliano?________________________________

iii. Ni latitude ipi inayoigawa dunia katikati katika kizio cha Kaskazini na Kusini_____

4)

i. Mtawanyiko wa watu katika uso wa dunia husababishwa na aina ya udongo, hali ya hewa, Uoto na sura ya nchi. Je hivi vipengeje vyote vipo katika sababu ipi_________________

ii. Elimu inayotumiwa na mwanahistoria kupata taarifa zinazohusu historian a utamaduni wa maisha kwa kuchunguza mila, desturi na lugha huitwa?_______________

iii. Masharika ya Umma yana mashamba makubwa ya kufugia Mifugo yanaitwa____________________


5) Ni aina ani ya ikabaila iliyokuwa imeshamiri sana katika maeneo yafuatayo.

i. Pwani __________________________

ii. Kanda ya ziwa.____________________

6) Taja nchi mbili zilipata uhuru kwa njia ya Mapinduzi barani Afrika.

i. _______________________ ii. ___________________________


A
B
C
D
E
F
G
H
I

**SEHEMU C (ALAMA 10)**

7. I ). Herufi J inawakilisha mto gani
   II). Taja shughuli za kiuchumi zinazoweza kufanyika Eneo A.
   III). Tanzania inapakana na nini upande wa Mashariki
   IV). Herufi C huwakilisha eneo gani la kihistoria.
   V). Ni aina gani ya kipimo inayo weza kutumika kuchora ramani hiyo

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA.

## MTIHANI WA MAJARIBIO YA MWEZI MACHI, 2024.

## SOMO: HISABATI.

MAELEZO

1. Mtihani huu una jumla ya maswali 8 yenye vipengele 33.
2. Jibu Maswali yote.
3. Onyesha njia kwa kila Swali kwa usahihi.

MUDA : MASAA 2:00.
SEHEMU A : MATENDO YA KIHISABATI (ALAMA 10)

| **NA.** | **SWALI** | **KAZI** | **JIBU** |
|---|---|---|---|
| | i. Jeni alikuwana tetea 54 139 na Majogoo 10 545. Je jumla alikuwa na Kuku wangapi? | | |
| | ii. ikiwa utapunguza 10 000 kutoka kwenye 350 960. Utabakiwa na ngapi? | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | iii. Selikari ilitoa mgao wa Vyandarua 32 52. Je, kila Kijiji kilipata Vyandarua vingapi, ikiwa kuna Vijiji vine? | | |
| | iv. Ukigawanya 7.15 kwa 0.013. Jibu litakuwa lipi? | | |
| | v. Tafuta zao la 66 767 na 300. | | |
| | vi. Ipi ni tofauti kati ya $6^{1}/_{2}$ na $3^{1}/_{5}$ | | |
| | vii. Tafuta jumla iliyopo kati ya 0.413 na 0.34. | | |
| | viii. Tafuta tofauti 5.43 na 2.998. | | |
| | ix. Tafuta hisa ya $4^{1}/_{2}$ na $1^{1}/_{4}$ | | |
| | x. Kokotoa thamani ya 3+4 (8-2) ÷6 | | |


**SEHEMU B: MAFUMBO (ALAMA 30**).


| NA | SWALI | KAZI | JIBU |
|---|---|---|---|
| 2 | i. Ipi ni thamani ya tarakimu 3 katika namba 1593945? | | |
| | ii. Vitabu 99000 viligawiwa katika shule 200 kwa idadiu sawa. Je, kila shule ilipata vitabu vingapi? | | |
| | iii. Ikiwa Juma alilipa TSH. 10,000 wakati alikuwa anadiwa Tsh. 8950. Je, alibakiwa na kiasi gani ? | | |
| | iv. Iwapo umepewa $2^{1}/_{2}$% katika maandishi, Je, ipi ni namba itakayo kuwa swan | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | a namba hiyo katika maandishi ya sehemu rahisi? | | |
| | v. | Iwapo kila tarakimu hutumika mara moja tu kati ya 3,7,9,6,8, na 1. Je, ni namba gani ndogo kabisa itakayoundwa? | | |
| | vi. | Ipi ni thamani ya tarakimu XXX katika XXX katika XXXVIII ? | | |
| 3 | i. | Iwapo John alitembea umbali wa meta 3.5 . Je, umbali huo ni sawa na sentimeta ngapi ? | | |
| | ii. | Toa tani 5 kilogramu 200 kutoka kwenye tani 7 na kilogramu 200. | | |
| | iii. | Zidisha kg 5 na g 250 kwa 8. | | |
| 4 | i. | Umri wa Jane ni miaka 5 zaidi ya umri wa Kemi . Jumla ya umri wao ni miaka 25. Tafuta umri wa Jane. | | |
| | ii. | Fikiria namba ,izidishe namba hiyo kwa 3 kisha jumlisha na 5 . Iwapo jibu ni 20 .Je, namba hiyo ni ipi? | | |
| | iii. | Watoto 5n +15 walikula machungwa 350 .Tafuta thamani ya n ikiwa kila motto alikula chungwa moja. | | |



| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | i. | Gharama za kukodi gari sh. 140, 000.Kokotoa gharama ya kukodi gari hilo kwa safari yenye umbali wa km 148. | | |
| | ii. | Juma aliwagawia watoto wake Asha, Baraka, na Ally kiasi cha shilingi 360,000 katika uwiano wa 1: 2: 3:.Je, Asha alipata kiasi gani cha fedha? | | |
| | iii. | Wafanyakazi 12 walivuna Heka 8 kwa siku 8. Wafanyakazi 18 wakiongezeka, watavuna shamba hilo kwa siku ngapi? | | |
| 6 | i. | Bei ya baiskeli imeongezeka kutoka laki tatu hadi laki nne na nusu . Tafuta asilimia ya bei iliyoongezeka. | | |
| | ii. | Bahati alinunua shuka 3 @ shilingi 5000 , mashati 2@ shilingi 3000, sahani 4@ shilingi 1000 na bakuli 5@ 500.Baada ya manunuzi hayo alilipa kiasi gani? | | |
| | iii. | Rashidi alimtembelea shangazi yake na kukaa nae kwa muda wa masaa 12:00. Je, saa hizo ni sawa na siku ngapi? | | |

**SEHEMU C: TAKWIMU NA MAUMBO**.

| NA | SWALI | KAZI | JIBU |
|---|---|---|---|
| 7 | i. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha namna Mzee Mbingwa alivyotumia mshahara wake wa shilingi 720,000. Je, hutumia kiasi gani cha fedha kwa chakula?<br><br> | | |
| | ii. Wastani wa alama 5 za wanafunzi ni 86% ikiwa masomo 4 alipata alama zifuatazo 92%, 85%, 88%, na 90%. Tafuta alama ya somo la tano. | | |

| NA. | SWALI | KAZI NA JIBU. |
|---|---|---|
| 8. | i. Ikiwa mzi ngo wa umbo hili n ism 26. Tafuta eneo lake.<br><br> | |
| | ii. Tafuta ujazo wa umbo hili katika lita. Ikiwa lita 1= $sm^3$ 1000 | |



| | | |
|---|---|---|
| |   | |
| | iii. Tafuta eneo la sehemu iliyotiwa kivuli ( $\pi=22/7$).   | |